

# **KAPSABET HIGH SCHOOL**

## **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. Mwanafunzi azingatie muundo wa wasifu;

### **Kichwa**

Kitaje wasifu ni wa nani, iandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari

### **Mwili**

Maelezo ya kibinagsi kuhusu anayesifiwa mfano majina yake kamili, alikozaliwa, alikosome, wazazi au familia yake n.k

Mambo mengine kumhusu ,matendo aliyotenda, ushindi wake n.k

### **Hitimisho**

Mwanafunzi ahitimishe kwa kutoa kauli ya mwisho kuhusu umaarufu wa anayeandikiwa wasifu na sababu za kuhitaji utambulisho.

Maudhui katika mwili wa insha yatiririke kiwakati

Wasifu uandikwe kwa wakati uliopita kwa sababu yanayosimuliwa huwa yamefanyika tayari.

Mwanafunzi atumie nafsi yan tatu umoja.

Wasifu uwe wa kuvutia kwa KUZINGATIA SABABU ZA MHUSIKA KUWA SHUJAA na kutoa mifano ya mambo maarufu yaliyotendwa na mhusika.

Mambo hasi ambayo yanaweza kumwathiri au kumwaibisha mhusika yaachwe.

### **TANBIHI**

Akitumia nafsi ya kwanza amepotoka apewe 03

Akitumia hotuba kama sura atuzwe maudhui na atolewe maki nne za sura

Maudhui yake yazingatie kwa nini mhusika ni shujaa

## **2 Mchakato wa kisiasa umeleta madhara mengi nchini. Jadili kauli hii.**

- Kiuchumi - umezorota
- ukabila–mauaji
- ukoloni mamboleo – wale wanaotawala wananyanya watu
- ukosefu wa miundomsingi
- utabaka – jamii kugawika
- uchochezi kupitia kwa wafuasi wa viogozi hasa vijana
- ufisadi – umekithiri kwa vile wezi wanafichwa
- uhalifu
- maendeleo kuegemea sehemu fulani za nchi na kusahau wengine
- ubadhinifu wa mali – hela nyingi kutumika kwa siasa badala ya kusaidia wananchi
- sera potovu

## **3 Hii ni insha ya methali; ukiona mahali kuna hatari /jambo linaloweza kukudhuru usikaribie**

Insha hii ina sehemu mbili;

Dudu liumalo - hatari ya aina yoyote ile

Silipe kidole – tahadhari

4 Kisa kioane na mdokezo uliopewa.

Kisa kisimuliwe katika nafsi yoyote

Lazima kisa kisimulie tendo / tukio ambalo msemajji alilionna na halikubaliki katika jamii yake kama vilemitindo ya mavazi, ulevi/dawa za kulevya, mahusiano yasiyokubalikahali ya anayerejelewa n.k.